

# HALMASHAURI YA MANISPAA KIGAMBONI

Simu: +255 22-2928468  
Fax: +255 22-2928469  
Barua pepe: info@kigamboni.go.tz  
Tovuti: www.kigambonimc.go.tz



S.L.P. 36009,  
KIGAMBONI,  
DAR ES SALAAM,  
TANZANIA.

## TAARIFA KWA UMMA

Baraza la madiwani la Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kwa pamoja leo limekasimia na kupitisha mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha **2019/2020** wenye jumla ya **Tsh. 35Bilioni** ambapo kati ya fedha hizo **Bilioni 30** ni ruzuku kutoka serikali kuu na wafadhili mbalimbali na **Bilioni 5** ni fedha za makusanyo ya ndani.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Halmashauri ya Kigamboni imekuja na bajeti inayojitosheleza inayolenga kufikia malengo ya miradi itakayopangwa kutekelezwa tofauti na makisio ya mwaka uliopita ambapo pia kupitia fedha za serikali kuu imejipanga kusimamia na kutekeleza kwa ukamilifu mradi wa ujenzi wa soko la kisasa la Kibada na kumalizia miradi viporo ili iweze kuleta tija kwa jamii na kuongeza pato la Manispaa kwa kuwa vyanzo vipya vya mapato.

Katika mwaka wa fedha **2018/2019** Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni inatarajia kukusanya/kupokea fedha kiasi cha **Shilingi Bilioni 35**. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 26**, ni Ruzuku kutoka Serikali Kuu na Wafadhili mbalimbali wa Maendeleo, **Bilioni 8** ni fedha za makusanyo ya ndani ya Halmashauri ambapo hadi sasa makusanyo ya ndani ni sawa na 45.38% asilimia.

**imetolewa na :**  
**kitengo cha Teknolojia Habari na Mawasiliano**  
**halmashauri ya manispaa ya kigamboni**  
**22/02/2019.**